

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

### TAARIFA YA TAFTISHI/UCHUNGUZI (INQUIRY)

- MADA:** Maombi ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya  
MOSHI ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake.
- TAREHE:** 13 Septemba 2007 Siku ya Alhamisi
- MUDA:** Saa 3:30 Asubuhi
- SEHEMU:** UKUMBI WA UHURU HOSTEL katika Manispaa ya  
MOSHI

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (yaani *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA)*), imepokea maombi ya **Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka ya Mji wa Moshi (MUWSA)** yenye kumbukumbu Nambari-TR-W-07-011 ya kutaka kurekebisha bei zake (*tariff*) za huduma za Maji safi na Maji Taka kuanzia **tarehe 1 Januari, 2008**.

Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414, EWURA itafanya mkutano wa kupata maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi kutoka kwa wadau wa mwombaji ili kujua uhalali wa maombi hayo ya kurekebisha bei za huduma zake.

EWURA imeandaa mkutano utakaofanyika katika Ukumbi wa Hostel ya UHURU mjini Moshi, siku ya **Alhamisi, tarehe 13 Septemba 2007**, kuanzia saa tatu na nusu asubuhi, ili kupata maoni ya wadau wakiwemo Baraza la ushauri la watumiaji wa huduma za maji (yaani *Consumer Consultative Council (CCC)*) pamoja na wadau wengine kuhusu ombi hilo la MUWSA. Wawakilishi wa MUWSA pia wamealikwa kwenye mkutano huo ili washiriki kwenye taftishi/uchunguzi huu.

Wananchi wanaopenda kushiriki katika taftishi/uchunguzi huu pia wanaalikwa kuhudhuria. Wale watakaoamua kushiriki kwa kutoa mada yao siku ya taftishi/uchunguzi watatakiwa kujisajili, kupata nakala ya hoja za **MUWSA** na kuwasilisha hoja zao kwa maandishi kabla ya saa 11 jioni mnamo tarehe **11 Septemba 2007 (Jumanne)**. Mshiriki atatakiwa kuchangia gharama za usafirishaji na za kudurufu makabrasha. **Makabrasha na nyaraka husika zinapatikana pia katika ofisi za MUWSA kwa Ofisa Uhusiano wa Mamlaka.**

Wadau wengine ambao wanapenda kutoa maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi huu wanakaribishwa kuleta maoni yao ki-maandishi na kuyatuma kwenye anuani iliyoonyeshwa hapa chini, kabla ya siku ya Alhamisi tarehe **27 Septemba, 2007.**

***Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Udhhibiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA),  
Ghorofa ya 6, Harbourview Towers (zamani JM Mall Building),  
Samora Avenue, P O Box 72175  
DAR ES SALAAM***